# OUP – Sera ya Faragha ya Kimataifa

| **Rekodi ya Historia ya Mabadiliko** | | | |
|---|---|---|---|
| **Toleo** | Tarehe ya Mabadiliko | Madhumuni | Mwandishi |
| **1** | 2018 | Toleo la kwanza | Timu ya Faragha |
| **1.1.** | Novemba 2022 | Mabadiliko madogo | O Ali |
| **1.2** | Machi 2023 | Mabadiliko madogo | M Kennedy |
| **2** | Machi 2023 | Idhini | J Patel |
| **2.1** | 07/09/2023 | Mabadiliko madogo | M Kennedy |
| **3.0** | 04/10/2023 | Idhini | J Patel |
| **3.1** | 24/11/2023 | Badilisha rights.requests@oup.com na DSR.Requests@oup.com | M Kennedy |
| | | | |

## 1. Utangulizi

1.1. Oxford University Press ("OUP") imejitolea kulinda taarifa zako za kibinafsi na kuheshimu sheria zinazotumika za ulinzi wa data ulimwenguni kote, ikiwemo, mahali inapotumika, Sheria ya Ulinzi wa Data ya Uingereza 2018, Kanuni Kuu ya Ulinzi wa Data ya Uingereza, Kanuni Kuu ya Ulinzi wa Data ya Muungano wa Ulaya (EU), Sheria ya Faragha ya Watumiaji ya California, Sheria ya Ulinzi wa Faragha ya Watoto Mtandaoni, na Sheria ya Haki za Elimu na Faragha ya Familia. Sera hii ya faragha inaelezea jinsi tunavyofanya hivyo na jinsi inavyohusika kwenye matumizi yako ya tovuti, bidhaa na huduma za OUP.

## 2. Jinsi tnavyotumia taarifa yako ya kibinafsi

2.1. Tunatumia taarifa ya kibinafsi ili kutangaza na kutoa bidhaa na huduma za OUP, kuhakikisha usalama wa tovuti zetu na kuendesha biashara yetu. Tumeweka kwenye ukurasa huu maelezo zaidi kuhusu aina ya taarifa za kibinafsi tunazokusanya, njia mahususi ambazo tunachakata taarifa hizo za kibinafsi, misingi ya kisheria inayoturuhusu kufanya hivyo na aina ya washirika ambao tunashiriki nao taarifa zako za kibinafsi.

2.2. Katika hali fulani ambapo tunaomba taarifa yako ya kibinafsi, tunafanya hivyo ili kutimiza ombi lako (kwa mfano, tunahitaji anwani yako ili tukutumie agizo lako). Iwapo hutatoa taarifa hiyo ya kibinafsi, hatutaweza kuchakata ombi au agizo lako.

2.3. Bila kujali jinsi tnavyotumia taarifa yako ya kibinafsi, tumeweka hatua ili kuhakikisha usiri, uadilifu na upatikanaji wake. Hii inajumuisha kutimiza kiwango cha ISO 27001, na utekelezaji wa mkusanyo wa mazoea ya usalama ya kiufundi na ya shirika ya kulinda data isipotee, kuibiwa au kutumiwa kwa njia isiyoidhinishwa. Kwa maelezo zaidi kuhusu ulinzi wetu wa OUP, unaweza kuwasiliana na privacy@oup.com.

## 3. Kutoa na kuondoa ridhaa na kubadilisha data yako ya kibinafsi

3.1. Pale ambapo ridhaa yako inahitajika ili tuchakate taarifa yako ya kibinafsi, tutaomba ridhaa yako wakati ambapo unatoa data yako. Una haki ya kuondoa ridhaa hiyo wakati wowote. Unaweza pia kubadilisha taarifa yako ya kibinafsi wakati wowote. Ukipenda

kufanya hivyo, unaweza kujaza Fomu yetu ya Ombi la Data ya Kibinafsi au uwasiliane nasi kupitia rights.requests@oup.com.

3.2. Hatuuzi taarifa yako ya kibinafsi kwa wahusika wa nje.

## 4. Kuhifadhi, kuhamisha na kuweka data yako ya kibinafsi

4.1. Taarifa yako ya kibinafsi inaweza kuhifadhiwa na kuchakatwa nje ya nchi ambapo inakusanywa, ikiwemo nje ya Uingereza ("UK") na Eneo la Uchumi la Ulaya ("EEA"). Tunapohamisha taarifa kwenda kwa wengine, ndani ya UK/EEA au vinginevyo, tunahakikisha kwamba kuna ulinzi na hatua za kiufundi zinazofaa ambazo zimewekwa ili kulinda taarifa yako ya kibinafsi. Ili kufanya hivyo, tutahamisha data tu kwenda katika nchi ambazo zimetambuliwa kuwa zinatoa ulinzi wa kutosha kwa taarifa za kibinafsi zinazotokea nchini Uingereza au kwenda kwa mhusika mwingine ambapo tumeweka mbinu zilizoidhinishwa za uhamishaji ili kulinda data yako ya kibinafsi. Kwa uhamishaji wa taarifa za kibinafsi kutoka UK/EEA, tunatumia mikataba ya kimataifa ya uhamishaji wa data, vifungu vya kawaida vya mkataba ambavyo vimeidhinishwa na Ofisi ya Kamishna wa Taarifa wa Uingereza na Tume ya Ulaya, tunatumia Sheria za Shirika za Lazima zilizowekwa na wagawaji wetu au tunatekeleza hatua nyingine kama hizo zinazohitajika kisheria ulimwenguni kote. Unaweza kupewa nakala ya mbinu husika ili uitathmini, iwapo utaiomba, kwa kutuma barua pepe kwa Ofisa wetu wa Ulinzi wa Data kwenye privacy@oup.com.

4.2. Tutaweka tu rekodi ya taarifa yako ya kibinafsi kwa muda mrefu kadiri inavyohitajika kwa madhumuni ambayo tumeikusanya na ili kuzingatia majukumu yoyote ya kisheria au ya udhibiti kuhusiana na uhifadhi wa rekodi. Tunaheshimu maombi ya kuacha kuchakata data yako ya kibinafsi kwa madhumuni ya masoko. Hii inajumuisha kuweka rekodi ya ombi lako kwa muda usiojulikana ili tuweze kuheshimu ombi lako katika siku zijazo.

## 5. Vidakuzi

5.1. Tunatumia vidakuzi kwenye tovuti zetu na teknolojia kama hizo katika programu zetu na programu nyinginezo. Tafadhali angalia Sera yetu ya Vidakuzi kwa maelezo ya jinsi hii inaweza kutumika kwako.

## 6. Haki Zako

6.1. Una haki ya kuomba ufikiaji na urekebishaji au ufutaji wa taarifa yako ya kibinafsi, haki ya kuzuia uchakataji wa taarifa yako ya kibinafsi na haki ya kupinga uchakataji wa taarifa yako ya kibinafsi. Una haki ya kupinga taarifa yako ya kibinafsi kuchakatwa kwa sababu za maslahi halali ya OUP. Una haki ya kupinga tusikutumie ujumbe wa masoko wa moja kwa moja na kukuainisha kwa madhumuni ya matangazo ya masoko ya moja kwa moja. Ikiwa ungependa kutumia haki yoyote iliyoelezewa, unaweza kujaza Fomu yetu ya Ombi la Data ya Kibinafsi au uwasiliane nasi kupitia rights.requests@oup.com.

6.2. Ikiwa una maswali yoyote kuhusu sera hii ya faragha, unaweza kuwasiliana nasi kupitia privacy@oup.com.

6.3. Una haki ya kutoa malalamiko dhidi ya uchakataji wetu wa taarifa yako ya kibinafsi kwa mamlaka ya usimamizi wa ulinzi wa data katika nchi unayoishi, kufanya kazi au ambapo

unaamini kuwa ukiukaji umetokea.

## 7. Kuwasiliana nasi

7.1. Mdhibiti wa data wa tovuti, bidhaa na huduma zetu ni Mkuu wa Chuo Kikuu, Walimu na Wasomi wa Chuo Kikuu cha Oxford, kinachofanya biashara kama Oxford University Press, ya Great Clarendon Street, Oxford OX2 6DP, Uingereza, isipokuwa kama imeonyeshwa vinginevyo kwenye tovuti, bidhaa, huduma au fomu ambayo kupitia hiyo umetupatia data yako ya kibinafsi. Kwa mfano, ikiwa ulitoa data yako ya kibinafsi kupitia tovuti ya www.oupe.es, mdhibiti wa data ni Oxford University Press España S.A. Ikiwa huna uhakika mdhibiti wako wa data ni nani au ikiwa una maswali mengine yanayohusiana na sera hii, Ofisa wa Ulinzi wa Data wa OUP anaweza kufikiwa kwenye anwani hiyo hiyo au kupitia barua pepe kwenye privacy@oup.com.